

Baadhi ya vijana wakitunukiwa shahada katika moja ya vyuo vikuu nchini. **Picha ya Maktaba.**

# Vijana wahitimu wawezeshwe kuwekeza nchini

**"Utafiti umebaini kwamba gharama za kuanzisha mradi mpya au ambao unaendelezwa ni Dola 100,000 za Marekani kwa wazawa na kwa wageni ni Dola 300,000 za Marekani.**

Veneranda Sumila, Mwananchi

Changamoto nyingi zinazozunguka mazingira ya ujasirimali nchini zinasababisha vijana wengi kushindwa kutengeneza miradi ya kujiajiri.

Utafiti umebaini kwamba changamoto nyingi ni za kifedha na zimewakwamisha wahitimu vijana kufanikisha malengo yao kwenye sekta ya uzalishaji mali au kutoa huduma.

Tafiti nyingi zilizofanywa zimebainisha kwamba kuna tatizo kubwa la upatikanaji wa fedha kama chanzo cha mtaji wa kuanzisha kazi ya kutoa huduma au kuzalisha mali.

Theluthi tatu za tafiti nyingi zilizofanywa kwenye ujasiriamali mdogo na wa kati zimesaidia kupata taarifa kwamba kikwazo kikubwa ni upatikanaji wa mtaji, fedha.

**Mtaji ni kikwazo kwa vijana**

Tatizo la upatikanaji wa fedha ndilo linasababisha vijana wakose uwezo wa kutekeleza ubunifu wa miradi kwenye ujasiriamali mdogo na wa kati (SMEs).

Taarifa za Chama cha Ushirika cha Wahitimu wa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (Sugeco), zilibainisha kwamba tatizo hilo ni kubwa zaidi kwa vijana wengi ambao wamehitimu shahada. Kwa mujibu wa taarifa hiyo taasisi za fedha hasa za benki, zinakupesha biashara ambazo zina faida na menejimenti zenye uzoefu na dhamana zinazouzika.

"Hii ni changamoto kubwa kwa wahitimu vijana ambao hawajapata fursa za kutengeneza dhamana zinazokubalika katika taasisi za fedha, wala kuwa na uzoefu wa masula ya mradi walioutekeleza," inasema sehemu ya taarifa ya utafiti huo ambao umedhaminiwa na taasisi ya BEST-AC.

Mchumi wa kilimo kutoka Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Revelian Ngaiza ameishauri Serikali kuwasaidia watu wanaotaka kuanzisha miradi mbalimbali kupata msaada wa kifedha kutoka taasisi za fedha nchini.

"Miradi midogo ni muhimu katika kustawisha uchumi, kama miradi hiyo itapatiwa fedha inaweza kabisa kubadili uchumi wa taifa hili," anasema Ngaiza.

Pia kutokuwapo kwa utamaduni wa kubuni na kutekeleza miradi ya ujasiriamali ni tatizo lingine kwa wanaotaka kuanzisha biashara za huduma au uzalishaji mali.

Utamaduni wa jamii kutambua, kuthamini kazi na kujituma katika ubunifu na utekelezaji wa miradi, ni tatizo.

"Vijana wapo katika mtego wa kutaka vitu vizuri daima na wakati mwingine kutumia njia za mkato kufikia mafanikio," anasema Ofisa Mtendaji Mkuu Taasisi ya Maendeleo ya Ujasirimali na Menejimenti (IMED), Dk Donath Olomi ambaye amefanya utafiti huu.

Amesema jamii inawaona wahitimu na wenye mahitaji ya ujasiriamali kama watu wa ngazi za juu na hawahitaji msaada na badala yake watoa misaada wanapenda fedha ama msaada uwafikie wananchi maskini moja kwa moja.

**NINI KIFANYIKE?**

**Ili kufanikisha kuanzishwa kwa miradi ya kilimo Tanzania yafutayo yafaa kufanyika:**

**-Wahitimu vijana wasaidiwe kuanzisha miradi katika hatua zote. Wapatiwe mitaji, maeneo ya kufanyia kazi, ardhi na mahitaji mengine ya msingi.**

**-Kupunguza vikwazo katika kupata kivutio cha uwekezaji kwa mujibu wa taratibu za TIC. Ni vyema vivutio hivyo vikawa wazi kwa vijana ili kupata mchanganuo.**

"**Wakati huohuo**, wahitimu wenyewe nao wanaona kwamba kuanza biashara ndogo si sawasawa na wanastahili kuanza na biashara kubwa," anaeleza Dk Olomi.

Changamoto nyingine inayowakwamisha wahitimu vijana ni kukosekana kwa miundombinu yenye tija.

Wakati ardhi inayofaa kwa kilimo nchini ni kubwa, maeneo hayo yana matatizo makuwa ya miundombinu kama ya usafiri, maji na nishati.

Hali hiyo imeelezwa kusababisha usumbufu mkubwa hata kwa wale ambao wana uwezo na wanaotaka kuanzisha miradi.

"Wazalishaji wengi wanakosa maeneo ya kufanyia kazi zao, Serikali za Mitaa nao hawatoi huduma zinazoridhisha za ardhi kwa matumizi mbalimbali. "Huduma muhimu kama umeme, simu, maji na barabara zipo kwa kiwango cha chini au hazipo, na kusababisha gharama za kuanzisha biashara au huduma kuwa ghali sana," inasema sehemu ya taarifa hiyo.

Dk Olomi anabainisha kwamba huduma za kuwezesha mazingira bora ya biashara ni chache kwa sababu hakuna uwezo, msukumo bora na pia hakuna hamu ya kutekeleza miradi rahisi.

"Watoa huduma za kibiashara wana uwezo mdogo wa kuwezesha ujasiriamali, masuala ya kiufundi na utaalamu wa kuhuisha. Wengi wao hawana ujuzi wala elimu na wamekuwa na majukumu ya kufunza au kushauri kitu ambacho wao wenyewe hawajafundishwa au kufanyia kazi," anasema Dk Olomi.

Dk Olomi pia amesema kuna tatizo la mifumo ya kisheria na kanuni ambayo si rafiki katika kuanzisha mradi wa uzalishaji au huduma.

Ingawa masuala ya kisheria na utawala katika kuanzisha biashara yameboreka katika kipindi cha miaka 10 iliyopita bado kuna vikwazo vingi na mabadiliko yanakwenda taratibu.

"Mchakato wa kuanzisha biashara na hata kupata leseni ni mgumu na wenye gharama kubwa. Muda mwingi unatumika kufuatilia leseni. Kutokana na sababu hiyo biashara nyingi hazisajiliwi," utafiti umebainisha.

Ngaiza amesema kutokana na mchakato kuwa mgumu na wenye mzunguko mrefu, wawekezaji wa kitanzania wanaoishi nchi za nje wanashindwa kurejea nyumbani kwa ajili ya kuanzisha miradi ya kilimo.

"Kuna mtu anaishi ughaibuni na ameomba ardhi kwa ajili ya kuwekeza kwenye kilimo miaka saba iliyopita, lakini mpaka leo hajapatiwa eneo la kuwekeza," anasema Ngaiza.

Kwa mujibu wa utafiti huo serikali za mitaa zinawajibika kuwasaidia vijana kutumia elimu yao ya chuo kikuu kuwapatia nyenzo na mahali pa kuwekeza.

"Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC) kinapaswa kushirikiana na serikali za mitaa kuhakikisha kwamba ardhi na maeneo ya uwekezaji yanapatikana kukidhi haja ya wajasiriamali wahitimu wa vyuo vikuu," utafiti umeshauri.

Kwa mujibu wa utafiti huo, ili kukabiliana na tatizo la kodi utekelezaji wa sheria na kupatikana kwa mahitaji na uwekezaji ni vyema kituo cha uwekezaji (TIC) kuanzisha kitengo cha kuwasaidia wahitimu wanaotaka kujiingiza katika shughuli za kilimo au biashara ya kilimo.

**Tujadiliane kupitia ujumbe mfupi SMS kwa 15774 ukianza na neno BIZ na kufuatia ujumbe wako. Ujumbe wako mfupi ni bure, hautozwi.**

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy
UKURASA HUU UNADHAMINIWA NA BEST-AC NA MWANANCHI